

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Taaluma Na. 1,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
18 Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
40404 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inapenda kuwataarifu wananchi kupuuza habari inayosambaa katika mitandao ya kijamii inayosema;

“Waziri wa Utumishi, Angellah Kairuki amesema, kama wewe umemaliza chuo kikuu lakini umri wako umevuka miaka 30 endelea kusubiri ajira. Sasa hivi tunachukua walio na umri chini ya miaka 30 kwani idadi yao ni kubwa zaidi.”

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Angellah J. Kairuki (Mb) hajasema maneno hayo. Hivyo, wananchi na wadau wengine mnataarifiwa kupuuza habari hiyo.

**Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora)**

11 Mei, 2017